JAMHURI YA KENYA

**WIZARA YA MAZINGIRA, MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA MISITU**

IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA

Dagoretti Corner, Ngong Road, P. O. Box 30259, 00100 GPO, Nairobi, Kenya

Simu: 254 (0) 20 3867880-7, 0724 255 153/4

Barua pepe: director@meteo.go.ke, info@meteo.go.ke

Twita @MeteoKenya

## 1.0 TAARIFA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA KWA MSIMU WA MASIKA MACHI-MEI, 2026

Kipindi cha mvua ya Machi-Mei ni kipindi cha mvua za masika katika sehemu nyingi nchini. Kiwango cha juu cha mvua (Zaidi ya mm 300) hunakiliwa maeneo ya Ziwa Viktoria, Nyanda za juu za Magharibi, Katikati na Kusini Mwa Bonde la Ufa. Vilevile, Mashariki mwa Bonde la Ufa (ikiwemo Nairobi) na mwambao wa Pwani.

Mtazamo wa hali ya hewa kwa msimu wa mvua za Masika (Machi–Aprili–Mei, MAM), 2026 **(umbo la 1),** unaonyesha kuwa mvua ya wastani hadi juu ya wastani inatarajiwa katika Bonde la Ziwa Victoria**,** Nyanda za Juu Magharibi mwa Bonde la Ufa**,** Nyanda za Juu Mashariki mwa Bonde la Ufa (ikiwemo Nairobi), pamoja na Kaskazini-magharibi mwa Kenya. Vilevile, mvua ya wastani hadi chini ya wastani inatarajiwa katika Nyanda za Chini za Kusini-Mashariki**,** Kaskazini-Mashariki**,** na baadhi ya sehemu za Kaskazini-magharibi mwa Kenya. Aidha, mvua iliyo chini ya kiwango cha wastani inatarajiwa katika eneo la Pwani.

Katika msimu huu, mgawo wa mvua katika maeneo mengi nchini unatarajiwa kuwa wa duni hadi wa kiwango cha wastani kimaeneo. Mwanzo wake unakadhiriwa kuwa wa wastani hadi wa kuchelewa katika baadhi ya maeneo (**umbo la 2**). Mvua hizi zinatarajiwa kukumbwa na vipindi vya ukame. Vilevile, dhoruba za mara kwa mara zinaweza kutokea katika baadhi ya sehemu za nchi. Kilele cha mvua kinatarajiwa kwenye mwezi wa Aprili katika sehemu nyingi nchini isipokuwa sehemu za mwambao wa Pwani ambapo kilele kinatarajiwa kuwa mwezi wa tano.

.

## 2.0 KIINI CHA MTAZAMO WA MVUA KIMAENEO

**Utabiri wa kina katika Msimu wa Mvua za Masika (Machi-Mei) 2026 ni kama ifuatavyo:**

**2.1. Ziwa Viktoria, Nyanda za juu za magharibi ya Bonde la Ufa na Kaunti za Katikati na Kusini ya Bonde la Ufa: (*Siaya, Kisumu, Homa Bay, Migori, Kisii, Nyamira, Uasin Gishu, West Pokot, Elgeyo Marakwet, Nandi, Kericho, Bungoma, Kakamega, Busia, Trans Nzoia, Vihiga, Laikipia (Laikipia Magharibi), Nakuru na Narok*).**
Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea kiwango cha mvua ya wastani mpaka zaidi ya wastani. Pia, kuna uwezekano mkubwa wa mvua za dhoruba za mara kwa mara kushuhudiwa katika sehemu nyingi za maeneo haya.

**2.2 Kaunti za Kaskazini Magharibi (*Turkana na Samburu*):** Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea kiwango cha mvua ya wastani mpaka zaidi ya wastani. Aidha, kuna uwezekano mkubwa wa mvua za dhoruba ya mara kwa mara kushuhudiwa katika sehemu chache za Kaunti hizi.

**2.3 Kaunti za nyanda za juu ya mashariki mwa Bonde la Ufa (Pamoja na maeneo ya Nairobi)**: (*Nyandarua, Laikipia, Nyeri, Kirinyaga, Murang'a, Kiambu, Meru, Embu, Tharaka-Nithi na Nairobi*): Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea kiwango cha mvua ya wastani mpaka zaidi ya wastani. Pia, kuna uwezekano mkubwa wa mvua za dhoruba ya mara kwa mara kushuhudiwa katika sehemu nyingi za maeneo haya.

**2.4 Kaunti za Kaskazini Mashariki (*Marsabit, Mandera, Wajir, Garissa na Isiolo*)**: Kiwango cha mvua maeneo haya kinatarajiwa kuwa cha wastani hadi chini ya wastani. Hata hivyo, kuna uwezekano mkubwa wa baadhi ya maeneo haya kupokea mvua za dhoruba za mara kwa mara.

**2.5 Kaunti za nyanda za chini za Kusini-Mashariki ya Kenya (*Machakos, Kitui, Makueni, Kajiado, Taita-Taveta na maeneo ya ndani ya Tana-River*):** Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea mvua ya wastani mpaka chini ya wastani. Vilevile, kuna uwezekano mkubwa wa maeneo machache sehemu hizi, kupokea mvua za dhoruba za mara kwa mara.

**2.6 Kaunti za Pwani (*Mombasa, Kilifi, Lamu Kwale na maeneo ya pwani ya Tana River*)**: Kaunti hizi zinatarajiwa kupokea mvua ya chini ya kiwango cha kawaida. Sehemu chache zinaweza kupokea mvua za dhoruba za mara kwa mara.

***KUMBUKA: Vichocheo kama vile vimbunga vya kitropiki na mzunguko wa Madden Julian (MJO) ambavyo vinaweza kutabiriwa kwa muda mfupi tu, vina uwezekano mkubwa wa kuhitirafiana na utabiri wa mvua za msimu kwa sababu haviwezi kunakiliwa mwanzoni mwa msimu. Kwa hivyo, ni muhimu kusawazisha utabiri huu na utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na idara hii wa siku, juma na hata mwezi zikifuatanishwa na jumbe fupi boresha, ripoti za ushauri na jumbe za athari pamoja na tabiri za wiki na mwezi za Kaunti. Utapata habari hizi kwa Ofisi za huduma ya hali ya hewa katika kila Kaunti nchini. Ni vyema kuwa tayari kufahamishwa.***

## 3.0 MATARAJIO YA TAREHE ZA MWANZO NA KIKOMO CHA MVUA ZA MASIKA 2026

### 3.1 Mwanzo, Kikomo na Mgao wa mvua za Masika msimu wa Machi-Mei, 2026

Utabiri wa mwanzo, mwisho, na mgao wa mvua hizi ulitokana na utafiti wa kina kwa "model" za kisayansi kuhusu Hali ya Hewa Duniani (GCMs models) pamoja na uchambuzi wa takwimu za miaka ya nyuma iliyokuwa na sifa zinazofanana na mwaka huu na inaonyeshwa kwenye Jedwali 1. Mwaka ulioonyesha ufanano na mwaka huu ulichaguliwa kuwa 2023. Mwanzo wa mvua za masika unatarajiwa kuwa wa kawaida mpaka wa kuchelewa kwenye maeneo mengi nchini.

### Tarehe za mwanzo na kikomo cha msimu

Tarehe za mwanzo na kikomo cha mvua za Masika katika Kaunti mbali mbali ni kama ifuatavyo:

**Jedwali 1: Tarehe za Mwanzo, Kikomo na Mgao wa mvua kimaeneo.**

| | Sehemu | Miazo | Kikomo | Hali ya Mgao wa Mvua |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Nyanda za juu Magharibi ya bonde la Ufa/Ziwa Viktoria, Katikati na Kusini mwa Bonde la Ufa** *(Bungoma, Trans Nzoia, Uasin Gishu, West Pokot, Elgeyo-Marakwet, Nandi, Kakamega, Vihiga, Bomet, Kericho, Kisii, Nyamira, Homa Bay, Migori, Siaya,* | Mvua itaendelea kuanzia mwezi wa Pili | Huenda ikaendelea hadi Juni | ya kuridhisha hadi nzuri |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | *Kisumu, Busia, Baringo, Nakuru, Magaharibi mwa Laikipia na Narok)* | | | |
| 2 | **Kaunti zilizo nyanda za juu mashariki mwa Bonde la Ufa Pamoja na Nairobi** *(Nyeri, Kirinyaga, Murang'a, Embu, Meru, Kiambu, Nyandarua, Nairobi na maeneo ya Mashariki mwa Laikipia)* | Wiki ya pili hadi ya tatu Machi. | Kuanzia wiki ya tatu mpaka ya nne Mei | ya kuridhisha hadi nzuri |
| 3 | **Kaunti za nyanda za chini za Kusini Mashariki** (*Kajiado, Kitui, Makueni, Machakos, Tana River na Taita Taveta),* | Wiki ya tatu hadi ya nne Machi | Wiki ya pili hadi tatu ya Mei | Duni |
| 4 | **Maeneo ya Kaskazini mwa Pwani** (*Lamu, Malindi, mwambao wa pwani ya Tana River, na Kilifi)* | Wiki ya pili hadi ya tatu Aprili | Huenda ikaendelea hadi Juni | Duni |
| 5 | **Maeneo ya Kusini mwa Pwani** *(Mombasa, Kwale)* | Wiki ya kwanza hadi ya pili Aprili | Huenda ikaendelea hadi Juni | Duni |
| 6 | **Kaskazini Magharibi**: (*Turkana, Samburu*) | Juma la nne la Machi hadi juma la kwanza la Aprili | Wiki ya tatu hadi ya nne ya Mei | Duni |
| 7 | **Kaskazini Mashariki** (*Wajir, Isiolo, Garissa, Mandera and Marsabit*) | Inatarajiwa kuanza kutoka juma la nne la Machi hadi juma la kwanza la Aprili. | Wiki ya tatu hadi ya nne Mei | Duni |

***KUMBUKA: Taarifa kuhusu mwanzo, mgao, na kikomo cha mvua hizi itatolewa mara kwa mara kupitia utabiri wa kila juma na kila mwezi kadri msimu unavyokaribia. Taarifa hizi zitatoa maelezo ya kina kuhusu mabadiliko na mwenendo wa mvua ili kuwafahamisha wadau ili kuwasaidia kufanya maamuzi kwa wakati unaofaa.***


## 4. UTABIRI WA HALI YA JOTO.

Hali ya joto inatarajiwa kuwa juu ya wastani katika maeneo yote ya nchi, huku uwezekano mkubwa zaidi ukitarajiwa katika sehemu za Bonde la Ziwa Victoria, m**a**eneo ya Pwani**,** Nyanda za Chini za Kusini-Mashariki, pamoja na sehemu za Kaskazini-Mashariki mwa Kenya, **Umbo la 3.**

## 5. ATHARI ZINAZOTARAJIWA KUTOKANA NA MVUA ZA MASIKA 2026

Msimu huu wa mvua za masika unatarajiwa kuwa wa manufaa kwetu na pia wa kusababisha athari kwenye sekta mbalimbali. Habari zaidi kuhusu athari kuu ambazo huenda zikatokea zitatolewa na wadau wa sekta husika.


***KUMBUKA: Ni muhimu kusawazisha utabiri huu na utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na idara hii wa siku, juma na hata mwezi zikifuatanishwa na jumbe fupi boresha, ripoti za ushauri na jumbe za athari pamoja na tabiri za wiki na mwezi za Kaunti. Utapata habari hizi kwa Ofisi za huduma ya hali ya hewa katika kila Kaunti nchini. Utabiri huu huwapa watumiaji wa bidhaa hizi hali halisi ilivyo ili kuweza kupanga mikakati kwa ufanisi kabla ya janga kutokea***




Edward Muriuki

**KAIMU MKURUGENZI WA IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA NCHINI KENYA**


**Viambatanisho:**




*Umbo la 1: Utabiri wa Mvua za Masika, 2026.*




*Umbo la 2: Mwanzo wa Mvua za Masika, 2026.*




*Umbo la 3: Utabiri wa Mtazamo wa joto msimu wa Masika, 2026.*